COUNTY MOCK EXAMS-STD 8
2016

KISWAHILI PAPER

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

GATUZI LA NAIROBI
MTIHANI WA MWIGO
DARASA LA NANE - MWAKA 2016
KISWAHILI

Muda: Saa 1 Dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

   NAMBA YAKO YA MTIHANI

   JINA LAKO

   JINA LA SHULE YAKO
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:

Katika karatasi ya maswali:

19. Kitenzi 'nawa' katika kauli ya kutendesha ni,
    A. nawika
    B. nawia
    C. navya
    D. nawisha

    Jibu sahihi ni C.

Katika karatasi ya majibu:

18. [A] [B] [C] [D] 19. [A] [B] [C] [D] 20. [A] [B] [C] [D] 21. [A] [B] [C] [D] 24. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 19. Kisanduku chenye herufi C ndicho kilichorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Karatasi hii ya maswali ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.

FUNGUA UKURASA

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Dawa za kulevya__1__pale na kwa yeyote__2__.Ajabu ni kwamba__3__wa dawa hizi ni watu__4__na wenye mamlaka katika jamii. Dawa hizi zina__5__kikubwa na anayeshiriki hawezi kukubali kuacha kwani__6__.Wauzaji wa mihadarati ni matajiri wenye uwezo mkubwa kifedha. kushindana nao ni kama kupiga__7__ ukuta kunakoumiza mkono wako bure.

Wengi wa hawa matajiri hutumia maskini__8__dawa hizi kwa malipo__9__. Dawa hizi huuzwa katika mitaa ya mabanda, katika ofisi na hata barabarabi tu!. Wauzaji ni__10__ya sungura kwani licha ya juhudi za serikali kuangamiza biashara hii haramu, bado inanawiri na kuota mizizi.

	A	B	C	D
1.	popote	kokote	mnomote	pote
2.	ule	wale	yule	huyo
3.	wezi	walaguzi	watumizi	wasambazaji
4.	bendia	wakwasi	wapuuzi	waheshimiwa
5.	pato	fedha	mapato	kipato
6.	bandu bandu huishia gogo	chovya chovya humaliza buyu	nchovya asali huishia kuchonga mzinga	tone na tone bahari huwa
7.	ngumi	mkono	kidole	kofi
8	kuuza	kuyauza	kuziuza	kuiuza
9.	bora	mzomzo	duni	ghali
10.	mfano	sembuse	ja	mithili

Kwanza__11__maneno umbayo ni__12__kuyatamka katika jamii fulani. Kuepukwa au kutotumiwa__13__kwa maneno hayo huyafanya kutoweka kutoka katika matumizi ya__14__. Baadhi ya msamiati unaochukuliwa kama mwiko ni__15__na sehemu nyeti katika miili ya watu au wanyama.

	A	B	C	D
11.	yapo	kuna	kunayo	yako
12.	ibura	mwiko	miko	bayana
13.	angalau	isipokuwa	ijapokuwa	aghalabu
14.	jamii	jamaa	familia	jumuia
15.	usiohusiana	unaohusiana	unaohusu	unayohusiana.

Kuanzia swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lifalo sahihi kulingana na maagizo.

16. Andika sentensi hii kwa usemi wa taarifa
"Umekula leo?" Mama aliuliza
A. Mama aliuliza kama amekula leo.
B. Mama alitaka kujua kama alikuwa amekula siku hiyo
C. Mama alitaka kujua kama amekula leo
D. Mama alitaka kujua kama angekula siku hiyo

17. Kanusha sentensi ifuatayo:
Kuimba kwake kumetufurahisha.
A. Kuimba kwake hakukutufurahisha
B. Kuimba kwake hatukufurahia
C. Kutoimba kwake hakujatufurahisha
D. Kutoimba kwake hakukutufurahisha

18. Wanaume waliooa dada wawili kutoka nyumba moja wanaitanaje?
A. Mavyaa B. Mitara
C. Mwamu D. Mwanyumba

19. Ni sentensi ipi sahihi kati ya hizi?
A. Ningalikusomesha ungepita
B. Ningalikusomesha ungelipita
C. Ningalikusomesha ungalipita
D. Ningelikusomesha ungalipita

20. Baada ya kupika pure nuuma atienda_____mikate
A. kuchemsha B. kuoka
C. kukaanga D. kunanika

21. Kati ya sentensi hizi ni ipi inayoonyesha -po- ya mahali?
A. Kamau alipoketi aliamza kusoma.
B. Alipewa zawadi alipopasi mtihani.
C. Alipoketi mtoto pataoshwa asubuhi.
D. Mama alipoonunua matunda alifungwa.

22. Ni ya ala hizi za mziki ipi haichezwi kwa kupuliza?
A. Udi B. Baragumu
C. Chivoti D. tarumbeta

23. Badilisha sentensi hii katika ukubwa wingi:
Kijiko kilichotumuliwa na mke wake kimevunjika
A. Majiko yaliyotumuliwa na majike yake yamevunjika
B. Majijiko yaliyotumuliwa na majike yao yamevunjika
C. Majijiko yaliyotumuliwa na jike lao yamevujika
D. Majiko yaliyotumuliwa na majike yao yamevunjika

24. Ni sentensi ipi iliyo na "KWA" ya kumiliki?
A. Wake kwa waume wa kijiji chetu wanakutana.
B. Juma atarithi sabini kwa mia ya mali ya kakake.
C.Mtaishi na kula kwa shangazi yenu tangu leo
D. Kwao hakuendeki madhali baba yenu ni simba.

25. Tegua kitendawili hiki:
Faiza akiniona ajificha.
A. kobe B. Mwezi
C. Kivuli D. Kinyonga

26. Tambua aina ya maneno yaliyopigwa mistari
Mtoto alimnunuliwa kiti kizuri sana kwa utiifu wake.
A. Kivumishi, kivumishi, kielezi

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

B. Kivumishi, kivumishi, nomino
C. Kivumishi, kielezi, nomino
D. Kielezi, kivumishi, kitenzi

27. Chagua mutungano sahihi wa sentensi hizi.
Mgonjwa haoni. Mgonjwa haskii
A. Mgonjwa haoni na hasikii.
B. Mgonjwa haoni maadamu hasikii
C. Mgonjwa haoni wala hasikii.
D. Mgonjwa haoni ingawa hasikii

28. Chagua sentensi inayoonyesha hali ya kutendesha.
A. Rais ametangaza vita dhidi ya ulanguzi wa mihadarati
B. Mchanja kuni aamekaza kamba ili kuni zisidondoke
C. Chakula hicho kilimtosha mtoto wa shangazi
D. Kumbe ni yaya amemliza mtoto wa Amina.

29. Ni ipi asilimia mbili nukta tatu?
A. 2.3% B. 200 3% C. 102.3% D. 2/3%

30. Chagua kifungu kilicho tofauti na vingine.
A. Alamsiki-Binuru B. Buriani-Buriani dawa
C. Pole-Asanti D. Hujambo-Sijambo

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40

Kijiji cha Rahatule kilikuwa maarufu sana kwa anasa. Watu wa kijiji hiki walijulikana kwa kupenda raha kupindukia. Ingawa walikuwa wachapa kazi, sehemu kubwa ya pato lao iliishia kwenye maeneo ya burudani kama vile katika mabaa na madanguro.

Jambo jingine hi kwamba katika kijiji hiki, palitokea binti mmoja aliyekuwa na aina mpya ya kileo alichouza kisirisiri. Kiliwavutia sana wanaume kwani kila wakati walitaka kumwona pembeni ili waki faidi kileo kipya. Walioonja waliishia kuwapelekea wake zao ambao walikifurahia bila kujua kilikuwa haramu.

Vijana wadogo waliposikia habari za kileo hiki na utamu wake, walifanya juu chini kuona kuwa walipata fursa ya kukionja . Mzee Karamka alikuwa na barobaro kwa jina Maraha na mjakazi aliyeitwa Sijali. Karamka alipitia pale na kupewa sehemu yake.

Babake Maraha alipofika akiwa mlevi, hakusita kumwita Sijali kwani mkewe alikuwa safarini kikazi. Alimshauri Sijali kukionja kileo kile kidogo na alipokatan, alimtishia kumwachisha kazi ndipo maskini binti wa watu akaridhia kuonja kwa madai kuwa iwe mara ya mwisho. Siku iliyofuata Sijali alimwita Maraha na kumshawishi kuonja kileo alichomwachia baba yake. Maraha aliona raha kweli.

Haukupita muda mrefu ikabainika kuwa kileo kile kilikuwa na madhara makubwa kwa mtumizi. Wote waliokitumia walianza kulalamika na walipopimwa, walipatikana na sumu fulani mwilini ambayo ilianza kuwaua polepole. Mke wa Karamka alipopata habari akaamua kuwaita madaktari kuipima familia yake. Ajabu ni kwamba ni binti yake tu aliyeonekana salama kwani kila mtu alikuwa na sumu ile mwilini.

Alipoulizа Maraha alikiri kuonjeshwa na Sijali baada ya kupewa ba babake, Mzee Karamka. Hata naye aliugua kwa kuambukizwa na mumewe. Jamaa nzima iliangamia kwa sumu ile Makini, binti yao aliyekataa kata kata kuwa bendera.

31. Kando na Mzee Karamka nyumba yake ilikuwa na idadi ya watu wangapi?
A. 5 B. 4 C. 3 D. 2

32. Kijiji cha Rahatule kilijulikana kwa sifa gani?
A. Ulevi chakari B. Raha chakari
C. Vileo chakari D. Madanguro chakari

33. Ni ipi si sahihi kulingana na habari uliyoisoma?
A. Mke wa Mzee Karamka aliaga
B. Bin wa Mzee Karamka ni Maraha
C. Sijali alikuwa binti wa Mzee karamka
D. Maraha alionja kileo cha sumu.

34. Kinyume cha neno kijakazi ni
A. kitwana B. yaya
C. mfanyikazi D. nokoa

35. Kulingana na taarifa kumwona pembeni inamaanisha
A. kumwona kwenye pembe
B. kumwona msalani
C. kumwona kando kando
D. kumwona kando

36. Ni nani aliyemwonyesha Maraha kileo cha sumu?
A. Sijali B. Karamka
C. Makini D. Rahatule

37. Vijana walio fanya juu chini walifanya nini haswa?
A. Walitumia kila mbinu kunywa kileo.
B. Walikimbia juu chini kutafuta kileo.
C. Walifanya juu chini kuramba kileo.
D. Walifanya juu chini kuona kileo.

38. Mzee Karamka alimtishia Sijali kazi
Hii ni kwa ila gani?
A. Ya kumtaka Maraha aonje kileo
B. Ya kumtaka aonjeshe wana Rahaule kileo
C. Ya kumtaka Sijali aonje kileo
D. Ya kumtaka aonjeshe aila nzima kileo

39. Neno burudani kama lilivyotumika kwenye ufahamu halimaanishi nini kati ya haya?
A. Madangurono B. Baani
C. Ulevini D. Michezoni

40. Ni kichwa kipi kinachofaa ufahamu uliosoma?
A. Bendera Hufuata Upepo
B. Ulevi Haulipi
C. Kila Kilevyacho si Tembo
D. Ulevi Unamfaidi Mlevi

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40

Chudi alifahamika katika idara ya mauzo alikofanya kazi. Alikuwa meneja wa mauzo katika kampuni aliyokuwa maarufu sana jijini. Lakini hakujulikana kutokana na nafasi yake ya kazi bali kutokana na wasifu wake. Daima alipenda kuvaa suti na kufunga tai zilizochukuana vyema na suti zenyewe lakini hakuwa na tabia hii zamani. Waliomjua kwa karibu wanasema kuwa alianza kuva suti mara tu aliporudi kutoka uingereza alikoenda kufanya kazi ya kujipiga msasa.

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Aliibwaga chini tabia yake ya hapo awali ya kuvaa mavazi ya rangi. Viatu vyake vilipigwa [illegible] sulu kiasi cha kuwa aina ya viroe.

Kazini nako alipandishwa madaraka. Kabla ya kuenda ng'ambo kujipiga msasa alikuwa naibu meneja wa mauzo. Sasa alipandishwa madaraka na kuwa meneja wa mauzo mwenyewe. Aidha alipewa gari zuri kaziri. Sasa Lakuwa akijiunga na wenzake tena kung'ang'ania usafiri wa matatu.

Wakati wa chakula cha mchana, wafanyakazi wa idara hiyo walikwenda kula kwenye kioski cha mzee Tisamo kilichokuwa mkabala na mahali pao pa kazi. Hapo zamani Chudi aliandamana na wenzake kunda kwenye kioski hicho kupata chakula. Lakini alipotoka uingereza alikuwa mtu mwingine kabisa. Alikuwa kama nyoka aliyejibambua gamba lake la zamani. Hakuwa Chudi yule watu waliyemzoea. La hasha! Alikuwa Chudi mwengine.

Siku moja mwenzake kazini alimwendea chudi, "si leo twende pahali petu pa kawaida?" Chudi alimwangalia akamuuliza, "wapi huko?" Yule mfanyakazi alifikiri labda Bwana Chudi alikua amesahau mahali walikozoe kula chakula cha mchana baada ya kutoka ng'ambo. "Si pale tu kwenye kioski cha mzee Tisamo.U'mepasahau mara mora moja hii?" Alisema mwezake.

Chudi alimpiga jicho tena halafu akaangua kicheko kikubwa huku akisema, "Bwana wee, mimi huko siendi tena Siku hizi nimepanda ngazi bwana. Wewe huoni hivyo? Mimi sasa huenda kwenye hoteli ya vizito kama mimi mwenyewe." Yule mwenzake alijiondokea kwenda zake na kumwacha Chudiaende kwnye hoteli yake. angepanda juu kipunga hafikii mbinguni Baada ya miezi kadhaa mambo yalianza kubadilika. Ingawa Chudi alidhani amesoma sana, lakini alisahau kuwa kulikuwa na vijana wengi waliokuwa wakiyaendeleza masomo ya juu. Walipopata maarifa ya kutosha walirejea kutoka masomoni na kushikilia nyadhifa mbalimbeli kwenye ofisi za serikali na kampuni. Ujuzi wao ulizidi ule wa bwana Chudi mara kadha. Haikuchukua muda kabla cheo chake kunyakuliwa. Sasa akawa naibu meneja. Lakini kabla ya miezi mitatu kupita nafasi yake ya naibu nayo ikanyakuliwa na kijana mwenye ujuzi zaidi. Ilibidi Chudi kurejea kwenye kazi yake ya zamani ya ukarani.

Aalijaribu juu chini kuendelea na maisha yake ya juu lakini akashindwa. Hotelini aliacha kwenda saa saba aliagiza aletewe chakula ofisini. Alidai alikuwa na kazi nyingi haya hakuyafanya kwa muda mrefu. Aaalisumbuka mpaka hatimaye akaamua kurudi kwa mzee Tisamo. Aalihakikisha kuwa ametangulia kabla ya wenzake kufika hapo ndipo abugie chakula chake na atokomee kabla hawajaingia lakini kwa bahati mbaya wenzake walimkuta hapo hapo. Yule jamaa aliyemwambia kuhusu hoteli ya vizito alimwona.Alipaza sauti na kuwamba, " Bwana Chudi karibu tena bwana. Hi ndiyo hoteli ya vizito wenyewe!" Wenzake walicheka kwa sauti ya juu. Bwana Chudi alitahayari.

41. Chudi alijulikana sana kutokana na
A. madaraka yake B.utanashati wake
C. sura yake nzuri D. kazi aliyofanya
42. Mara ya kwanza Chudi alipandiswa
A. kabla ya kwenda ng'ambo
B. akiwa ng'ambo
C. badada ya kutoka ng'ambo
D. hakupandiswa madaraka
43. Kulingana na habari hii ni dhahiri kuwa maisha na wengi wa wafanyakazi walikuwa
A. mabwenyewnye
B. wakwasi
C. walalaheri
D. walalahoi
44. "Mimi sasa huenda kwenye hoteli ya vizito...."Usemi huu unamaanisha nini?
A. Hoteli ya watu wa uzani wa juu
B. Hoteli ya watu matajiri
C. Hoteli ya vyakula vizito vizito
D. Hoteli ya ya ghorofa
45. Ni methali gani haidhihirishi maana katika habari hii?
A. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba
B. Mpanda ngazi hushuka
C. Usione kasimama angalia usianguke
D. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi
46. Ina maana gani kusema kuwa Chadi alikuwa amekwenda ng'ambo kujipiga msasa?
A. Alikuwa ameenda kujiendeleza kimaarifa
B. Alikuwa ameenda kubadili mavazo yake
C. Alikuwa ameenda kuboresha masomo yake
D. Alikuwa ameenda kujifunza jinsi ya kuvaa mavazi ya kisasa
47. Manufaa aliyoyapata Bwana Chudi pale kazini baada ya kutoka uingereza yalikuwa gani?
A. Alianza kuvaa suti na tai zilizochukuana vyema
B. Alipandishwa cheo na kupewa gari zuri
C. Alikuwa kama nyoka aliyejibambua gamba lake la zamani.
D. Aliweza kuagiza kuletewa chakula ofisini kutoka hotelini
48. "Bwana Chudi karibu tena bwana. Hii ndiyo hoteli ya vizito wenyewe.".Ilikuwa ya
A. kufia uchungu
B. kumkera Bwana Chudi
C. kumwonyesha Chudi wamemuona mle ndani
D. Kumcheka Chadi
49. Kulingana na taarifa hii ni sifa ipi bora zaidi
A. Kubadilisha mahali pa maakuli
B. Chudi kuwa msomi
C. Chudi kuvaa suti na viatu vizuri
D. Chudi kuwa na gari la kifahari
50. " Kioski cha Bw. Tisoma kilikuwa mkabala wa kazini pao Chudi" ina maana.
A. kioski kilikuwa kando na kazi
B.kioski kilikuwa kando ya kazini
C. kioski kilitazamana na kazini
D. Kioski kilikuwa katikati

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27